JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA
Barabara ya Kitekele , S.L.P 81, Bukoba,
Simu: +255 (0) 282221744 Nukushi: 0282221588
Barua pepe: info@buwasa.go.tz Tovuti: www.buwasa.go.tz

# MKATABA WA AJIRA YA MUDA MFUPI YA UJENZI WA TENKI LA TOFALI ZA ZEGE LA KUHIFADHIA MAJI KWENYE MNARA WA MITA 6 LENYE UJAZO WA LITA 135,000 ZABUNI NA.AE/031/2021-2022/W/02/LOT-3 KATIKA MRADI WA MAJI KARABAGAINE ULIOPO WILAYA YA BUKOBA

**MKATABA HUU** unafanyika leo Tarehe .12., Mwezi ........11.........., 20..2021

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA (BUWASA),** S.L.P 81, (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri au BUWASA") kwa upande mmoja;

**NA**

**FUNDI DOMISIAN TEMARILWA BAGENZI WA** S.L.P ,284 Bukoba (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

**AMBAPO:**

a) Mwajiri ni tasisi ya serikali yenye jukumu la kutekeleza utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira Bukoba na yenye makao makuu yake Bukoba Mjini barabara ya Kitekele.

b) Mwajiriwa ni fundi binafsi anayejishughulisha na kazi za ujenzi katika mkoa wa Kagera mwenye makazi katika mtaa wa Kisindi-Bukoba.

c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa siku sabini na tano (75)

d) Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kama fundi wa kujenga Tenki la tofali za zege kuhifadhia maji la juu ya mnara wa mita sita(6) na kwa mujibu wa mchoro na kazi zingine kama zilivyo ainishwa katika kotesheni ya zabuni ya nukuu ya bei aliyojaza.

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA** kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

## 1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya **ujenzi wa Tenki la tofali za zege la kuhifadhia maji juu ya mnara wa mita sita(6) lenye ujazo wa lita 135,000** ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo:

a) **Kufanya kazi mtambuka zinazo endana na ujenzi wa Tenki lengwa kama zilivyo ainishwa katika mchoro na kotesheni ya zabuni ambayo amejaza nukuu za bei.**

## 2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku **sabini na tano (75),** ambapo itaanza tarehe ....12/11/2021.... na itakamilika tarehe ....7/02/2022....

## MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha **Tshs 18,413,220.00 (Milioni kumi na nane Laki nne Kumi na tatu elfu Mia mbili na ishirini tu.)** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;
b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);

c) Malipo hayo yatalipwa aidha kwa fedha taslim au hundi ambayo italipwa benki kupitia akaunti namba..............................;
d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu kadiri ya mwajiriwa atakavyotelekeza kazi alimradi kiasi kinachoombwa kisichopungua asilimia kumi (10%) ya mkataba huu.
e) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

**3. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI**

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kutoa maelekezo na kuonesha eneo la kazi;
b) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi;
c) Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Jumuiya ya Watumia Maji katika shughuli za ujenzi wa Mradi;
d) Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi ata mtaarifu fundi wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano
e) Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

**4. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA**

Mwajiriwa ambaye ni fundi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza ujenzi wa kazi zote kama zilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya Mkataba) kulingana na ramani na vipimo viliyotolewa na Mwajiri;
b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi atakaoujenga;
c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;
d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (*Project Manager*) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;

e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;
f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kila zitakapohitajika;
g) Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na
h) Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

**5. HAKI NA WAJIBU WA JUMUIYA YA WATUMIA MAJI/WANANCHI**

Jumuiya ya Watumiaji Maji itakuwa na wajibu na majukumu ya fuatayo:

a) Kushiriki katika kazi ndogo ndogo za kujitolea kwa ajili ya kushirikiana na mafundi;
b) Kutekeleza majukumu mengine pale inapohitajika kwa maelekezo ya Msimamizi wa Mradi; na
c) Kulinda vifaa vya ujenzi, mitambo na mradi wenyewe ili usihujumiwe.

**6. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO**

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (*casual labourers*) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

**7. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI**

Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, Mkataba wa Mwajiriwa utasitishwa ili kutafuta fundi mwengine. Mwajiriwa atakayekuwa ameshindwa kumaliza kazi kwa muda ulipongwa bila ya sababu za msingi atakuwa amejifuta kwenye kazi za ujenzi wa miradi ya maji ya BUWASA.

**8. DHAMANA YA UHARIBIFU**

a) Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na
b) Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.
c) Endapo utatokea wizi wa vifaa au uharibifu utakaofanywa na wewe mwenyewe au wasaidizi wako utawajibika kulipa gharama na faini itakayotokana na usumbufu wowote.

**9. SHERIA ITAKAYOTUMIKA**

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

**10. USULUHISHI WA MGOGORO**

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na

b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

**11. KUSITISHA MKATABA**

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

**12. MAREKEBISHO YA MKATABA HUU**

Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

**13. MASHARTI YA NYONGEZA**

Masharti mahsusi ya nyongeza kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:

a) Kulipa kodi ya serikali
b) Kuepusha migogoro inayoweza kuzuilika
c) Kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wanaojenga mradi

**KWA USHUHUDA HUU**, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

| **KWANIABA YA MWAJIRI (BUWASA)** | **Shahidi:** |
| --- | --- |
| **Jina:** CLAVERY T' CASMIR | **Jina:** YAZIDI BWIKIZO |
| **Sahihi:** K.n.y MKURUGENZI MTENDAJI<br>MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA<br>S.L.P. 81 BUKOBA | **Sahihi:** ................................ |
| **Cheo:** Mkurugenzi Mtendaji | **Cheo:** Meneja Ufundi |

| | |
|---|---|
| **Tarehe:** 12/11/2021 | **Tarehe:** 12/11/2021 |

| | |
|---|---|
| **KWANIABA YA MWAJIRIWA (FUNDI)** | **Shahidi:** |
| **Jina:** DOMISIAN TEMALIRWA | **Jina:** ANANIAS JUVENARY |
| **Sahihi:** ........................ | **Sahihi:** ........................ |
| **Cheo:** FUNDI | **Cheo:** FUNDI |
| **Tarehe:** 12/11/2021 | **Tarehe:** 12/11/2021 |

# KIAMBATISHO I

# KOTESHENI YA BEI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI**
**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA**
Barabara ya Kitekele, S.L.P 81, Bukoba,
Simu: +255 (0) 282221744 Faksi: 0282221588
Barua pepe: info@buwasa.go.tz Tovuti: www.buwasa.go.tz

20/10/2021

M/s DOMISIAN TEMALIRWA
BAGENZI
..........................................................

# NUKUU YA BEI: UJENZI WA TENKI LA MAJI LENYE UJAZO WA LITA 135,000 LA MAWE KWENYE MNARA WA MITA SITA(6) ZABUNI NAMBA AE/031/2021-2022/W/02/LOT-3

Tunapenda kukujulisha kwamba unaalikwa kufika ofisi za Mamlaka ya Maji safi na usafi wa mazingira Bukoba katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi kuchukua zabuni ya kujaza nukuu ya bei ya kazi ya ujenzi kama ilivoelezewa hapo juu katika eneo la Karabagaine.Unatakiwa kuwasilisha nukuu zako za bei pamoja **viambatisho vya nakala ya kitambulisho cha taifa/mpiga kura/leseni ya gari/passport, TIN certificate na barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa**. Waslisha nukuu za bei zikiwa zimefungwa kwa lakiri*(seal)* kwenye bahasha ilio andikwa **"UJENZI WA TENKI LA MAJI LENYE UJAZO WA LITA 135,000 LA MAWE KWENYE MNARA WA MTA SITA KATIKA MRADI WA MAJI- KARABAGAINE"** katika ofisi ya Ununuzi BUWASA. **Mwisho wa kuwasilisha ni 27/10/2021 saa tano (5) asubuhi**. Nukuu za bei tajwa hapo juu zitafungiliwa baada ya saa tano (5) kamili asubuhi katika ofisi za Ununuzi na mnakaribishwa kuhudhulia ufunguzi huo.

| NA | MAHITAJI | IDADI | KIPIMO | KIASI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| A | ~~UJENZI WA BPT YA 10M3~~ | | | | |
| 1.0 | Kusafisha na kuchimba eneo la kazi | 100 | m2 | 4000/= | 400,000/= |
| 1.1 | Kuhamisha vipimo kutoka kwenye mchoro hadi kwenye eneo la kazi (setting out) | 1 | L/sum | 100,000/= | 100,000/= |
| 1.2 | Kuchimba msingi wa kujenga tank la maji wenye kina kisichopungua 0.5m | 44.2 | M3 | 5000/= | 221000/= |
| 1.3 | Kusawazisha eneo la msingi | 36.83 | M2 | 5000/= | 184150/= |
| 1.4 | Kuandaa na kumwaga zege la kusawazisha (Blinding) | 1.84 | M3 | | 184000/= |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ..5 | Kutayarisha mbao na kufunga formwork | 36.83 | M2 | 5000/= | 184150/= |
| 1.6 | Kusuka na kulaza nondo za msingi wa tanki(Tank Foundation) | 36.83 | M2 | 5000/= | 184150/= |
| 1.7 | Kumwaga zege la msingi(Foundation) | 18.93 | M3 | 100,000/= | 1,893000/= |
| 1.8 | Kufunga formwork za column | 10.35 | M3 | 5000/= | 51,750/= |
| 1.9 | Kusuka nondo za Colum | 2 | M3 | 20,000/= | 60,000/= -40,000 |
| 2.0 | Kumwaga zege la Colum | 2 | M3 | 100,000/= | 200,000/= |
| 2.1 | Kujenga Matofari ya Msingi(Foundation Walls) | 25.81 | M2 | 20,000/= | 516,200/= |
| 2.2 | Kupanga mawe ya msingi (hardcore) | 8.75 | M3 | 20,000/= | 175,000/= |
| 2.3 | Kurudishia udongo na kushindilia kwa kutumia mashine(Compactor) | 16.2 | M3 | 30,000/= | 486,000/= |
| 2.4 | Kumwaga zege la Blinding kuzunguka msingi. | 1.84 | M3 | 100,000/= | 184,000/= |
| 2.5 | Kujenga kuta za matofari ya mnara kulingana na mchoro | 112.1 | M2 | 20,000/= | 2242000/= |
| 2.6 | Kufunga formwork za Beam | 5.72 | M3 | 10,000/= | 57200/= |
| 2.7 | Kusuka nondo za Beam | 5.72 | M3 | 20,000/= | 114400/= |
| 2.8 | Kumwaga zege la Beam | 5.72 | M3 | 50,000/= | 286,000/= |
| 2.9 | Kufunga vitanda kwa ajili ya kujengea Mnara wa Tanki | 1 | L/sum | 400,000/= | 400,000/= |
| 3.0 | Kufunga formwork za kitako cha Tanki | 32.10 | M2 | 10000/= | 321000/= |
| 3.1 | Kusuka nondo za kitako cha Tanki | 32.10 | M2 | 10000/= | 321000/= |
| 3.2 | Kumwaga zege la kitako cha Tanki | 9.6 | M3 | 100,000/= | 960,000/= |
| 3.3 | Kujenga kuta za Tanki kwa matofari | 74.96 | M2 | 50,000/= | 4497,600/= 3748,00 |
| 3.4 | Kusuka nondo za Colum ya ndani ya Tanki | 6.816 | M2 | 10000/= | 68160/= |
| 3.5 | Kufunga formwork za colum ya ndani ya Tanki | 6.816 | M2 | 10000/= | 68160/= |
| 3.6 | Kumwaga zege la colum ya ndani ya Tanki | 0.68 | M3 | 100,000/= | 68,000/= |
| 3.7 | Kupiga lipu kuta za tanki pamoja na mnara wa Tanki | 416.42 | M2 | 5000/= | 2,082,100/= |
| 3.8 | Kufunga scafford na formwork za kitako cha tanki | 1 | L/sum | 100,000/= | 100,000/= |
| 3.9 | Kusuka nondo za Mfuniko | 32.10 | M2 | 10000/= | 321,000/= |
| 4.0 | Kumwaga zege la mfuniko wa Tanki | 3.2 | M3 | 100,000/= | 320,000/= |
| 4.1 | Kufanya finishing za tanki | 208.2 | M2 | 2000/= | 416,400/= |
| 4.2 | Kufunga viungio vya maji na kujenga valve chamber | 3 | No. | 100,000/= | 300,000/= |
| 4.3 | Kupaka rangi tanki | 208.2 | M2 | 2000/= | 416,400/= |
| 4.4 | Gharama za maji ya kujengea | 1 | L/sum | 400,000/= | 400,000/= |
| 4.5 | Gharama za kusafirisha vifaa toka store hadi site | 1 | L/sum | 400,000/= | 400,000/= |
| | **JUMLA KUU** | | | | 19,182,820/= |

18,413,220/=

**MUHIMU**

i. Muda wa kukamilisha kazi hii ni siku 75 tangu kukabidhiwa eneo la kazi(site)
ii. Tenki linalotakiwa kujengwa ni la ujazo wa lita 135,000 la mawe kwenye mnara wa mita sita(6)
iii. Hakikisha unaweka viambatanisho vyote vinavyotakiwa kama vilivyo orodheshwa hapo juu.

Imewasilishwa na:

Jina la fundi DOMISIAN TEMALIRWA Saini [signature] Tarehe 28/10/2021

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA**

# KIAMBATISHO 2

# BARUA YA UKUBALI WA KUFANYA KAZI JATWA

DOMISIAN TEMALIRWA

S L P 517

BUKOBA

18/11/2021

BUWASA

S.L.P 81

BUKOBA

YAH KUKUBALI KAZI YA UJENZI WA KUJENGA TENKI LA MAJI LENYE UJAZO WA LITA 135000 LA TOFALI ZAZEGE ZABUNI NAMBA AE/031/2021-2022/W/02 LOT 3

Rejea kichwa cha habari hapo juu. Nina Furaha kuwajulisha kwamba nakub li na nitatekeleza kazi tajwa hapo ju Kama masharti ya mkataba unavyo sem Natanguliza Shukurani na subili kule kelezaji wa mradi wa maji tajwa hapo juu

Nimimi DOMISIAN TEMALIRWA


# KIAMBATISHO 3

# BARUA YA UTAMBULISHO NA KITAMBULISHO

# HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA

OFISI YA MTAA,
MTAA KISINDI,
S.L.P 284,
**KASHAI.**
TAREHE 29/10/2021

KUMB. NA. BMC/KSH/KS/ /
KWA, Mkurugenzi Ofisi
ya Manunuzi
Buwasa



MWENYEKITI WA MTAA KISINDI KATA KASHAI
P.O BOX 218
0755 302129
0784 302129
TAR.........
BUKOBA MANISPAA MKOA KAGERA

**YAH: UTAMBULISHO WA NDUGU Domisiani Temarilwa Bagenzi WA MTAA KISINDI KATA KASHAI.**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

Namtambulisha kwako mtajwa na mwenye picha iliyo bandikwa na kugongwa mhuri hapo juu kuwa ni Mkazi wa Mtaa Kisindi Kata Kashai Manispaa Bukoba.

Hivyo kwa barua hii naomba apewe huduma anayoomba.

Wako katika ujenzi wa Taifa.

.........[signature].........

MWENYEKITI WA MTAA KISINDI KATA KASHAI
P.O BOX 218
0755 302129
0784 302129
TAR.........
BUKOBA MANISPAA MKOA KAGERA

# DRIVING LICENCE
THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



1 Family name
BAGENZI
2 Given names
DOMISIAN TEMALIRWA
3. Date of birth
23/09/1976
4a Date of issue
27/03/2021
4b Date of expiry
18/02/2026
4c Issuing authority
TANZANIA REVENUE AUTHORITY
8 Permanent place of residence
Kagera
9 Categories of Vehicles
A B D
7 Signature

4d

Licence number
4004966376

0390633183

| 9. Categories of vehicles | 10. Date of issue | 11. Date of expiry |
|---|---|---|
| A | 20/02/2018 | 18/02/2026 |
| A1 | | |
| A2 | | |
| A3 | | |
| B | 20/02/2018 | 18/02/2026 |
| C | | |
| C1 | | |
| C2 | | |
| C3 | | |
| D | 20/02/2018 | 18/02/2026 |
| E | | |
| F | | |
| G | | |

4004966376

# KIAMBATISHO 4

# NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPA KODI( TIN NUMBER)

CTIN.

2392721

TRA

# TANZANIA REVENUE AUTHORITY

## CERTIFICATE OF REGISTRATION
## FOR
## TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER (TIN)

(ISSUED UNDER SECTION 23 OF THE TAX ADMINISTRATION ACT 2015)

## THIS IS TO CERTIFY THAT

**DOMISIAN TEMALIRWA BAGENZI**

HAS BEEN REGISTERED WITH THE TANZANIA REVENUE AUTHORITY AND ASSIGNED THE TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER

**135-848-247**

WITH EFFECT FROM: **13 January 2020**

TRA LOCATION: KAGERA TAX OFFICE: BUKOBA

PHYSICAL LOCATION:

STREET / AREA: KISINDI KASHAI

For Non Business Use Only

ABDUL Y. MAPEMBE

OFFICIAL SEAL AG. COMMISSIONER FOR DOMESTIC REVENUE

NOTE: THE REQUIREMENTS UNDER WHICH THIS CERTIFICATE IS ISSUED ARE STATED OVERLEAF